WIZARA YA ELIMU,
SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# MoEST Weekly

25 Februari, 2026




## 10 WAPATA UFADHILI SHAHADA YA UZAMILI KATIKA SAYANSI YA TAKWIMU NA AKILI UNDE KUPITIA SAMIA SCHOLARSHIP EXTENDED (SSE DS/AI+)

# 10 WAPATA UFADHILI SHAHADA YA UZAMILI KATIKA SAYANSI YA TAKWIMU NA AKILI UNDE KUPITIA SAMIA SCHOLARSHIP EXTENDED (SSE DS/AI+)

Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeanza kutoa ufadhili wa masomo ya Shahada ya Uzamili katika Sayansi Takwimu (Data Science), Akili Unde (Artificial Intelligence) na Sayansi Shirikishi kupitia mpango wa Samia Scholarship Extended (SSE DS/AI+).

Hatua hiyo imeanza kwa wanafunzi 10 waliopata ufadhili wa kusoma katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST) iliyopo Arusha. Aidha, wanafunzi wengine 10 wanatarajiwa kusoma masomo hayo katika Indian Institute of Technology Zanzibar IIT Madras kampasi ya Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Adolf Mkenda, amesema uamuzi wa kusomesha wanafunzi hao katika ngazi ya Uzamili unatokana na mahitaji ya taifa katika eneo la teknolojia na ubunifu. Amesema Serikali imetenga Shilingi bilioni 5 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo.

"Vyuo tunavyopeleka wanafunzi wa Samia Scholarship AI/DS+ vinatoa mafunzo kwa vitendo katika makampuni makubwa ya teknolojia, na vinaendelea kudahili wanafunzi wetu," amesema Prof. Mkenda.

Amefafanua kuwa wanafunzi waliopata ufadhili wanatoka katika shule za Serikali na zisizo za Serikali. Kwa ngazi ya Uzamili, waombaji huchaguliwa kupitia mfumo wa maombi, tofauti na ngazi ya Shahada ya Kwanza ambapo wanafunzi huchaguliwa kulingana na ufaulu wao wa juu.

Waziri Mkenda ametumia fursa hiyo kuwaalika wadau mbalimbali kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kuchangia mfuko wa Samia Scholarship, akisisitiza kuwa Serikali imeamua kuongeza nguvu katika masomo ya STEM (Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati).

Amesema juhudi hizo zinaonekana kupitia ujenzi wa shule maalum za wasichana za sayansi katika kila mkoa, upendeleo wa mikopo kwa wanafunzi wa sayansi kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, pamoja na utoaji wa ufadhili kupitia Samia Scholarship kwa wanafunzi waliomaliza Kidato cha Sita.







Prof. Mkenda pia amewataka wanafunzi waliopata ufadhili ngazi ya Shahada ya Kwanza kuangalia majina yao katika tovuti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia www.moe.go.tz, Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) *http://www.costech.or.tz* na Taasisi ya Afrika ya Sayansi ya Teknolojia ya Nelson Mandela *http://www.nm.aist.ac.tz*

Kwa upande wake, Makamu Mkuu wa NM-AIST, Maulilio Kipanyula, amesema mpango wa Samia Scholarship Extended (SSE DS/AI+) ni uwekezaji wa kimkakati unaolenga kujenga uwezo wa wataalamu wa ndani, huku ukitoa fursa ya wanafunzi kubadilishana uzoefu kimataifa kutokana na hadhi ya taasisi hiyo.